



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA ZA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**



**Kumb.Na KMC/L.40/8/131**

**03 Julai, 2024**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Manispaa Kahama imepata idhini ya utekelezaji wa Ajira Mpya katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa barua yenyewe Kumb. Na. FA. 97/288/01/09 ya Tarehe 25 Juni, 2024 kutoka kwa Katibu Mkuu ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora.

Hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anawatangazia Watanzania wenyewe Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi za hiyo.

**1.0 DEREVA DARAJA LA II- NAFASI (03)**

**1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha Sita (VI) na awe na ufaulu wa daraja la nne na kuendelea, awe mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani, awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari ( Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA**

- i. Kukagua Gari kabla na baada ya Safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za Kikazi
- iii. Kukusanya na kusambaza Nyaraka mbalimbali
- iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika Daftari la Safari
- v. Kufanya Usafi wa Gari.

### **1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali Ya **TGS B** kwa mwezi

### **1.0.4 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si Zaidi ya Miaka **45** na sio pungufu ya Miaka **18**.
- ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.
- iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.
- v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa
- vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- vii. Waomabji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni
- viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 17 Julai, 2024.
- x. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,

Barabara ya Boma,

S.L.P 472,

**KAHAMA – Shinyanga**

- xi. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye Mfumo wa Kieletroniki wa Ajira (**Recruitment Portal**) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.ajira.go.tz/> anuani

hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Secretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa "**Recruitment Portal**"

- xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili  
**HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na;

**MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA MANISPA**

**KAHAMA**